**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA YA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(OWM-TAMISEMI)**

**SHULE YA SEKONDARI LUPALILO,**
**S.L.P 51,**
**MAKETE**
**13/05/2026**

. . i

Makamu mkuu wa shule +255757423403 Mwalimu wa Bweni +255759374957
Mwl wa Taaluma +25575765268478

**Tovuti yetu www.lupalilohighschool.sc.tz**
**Namba za simu:**
**Mkuu wa shule +255755633995**
**Makamu mkuu wa shule +255757423403**

NDUGU MZAZI/MLEZI WA

**Mwalimu wa Bweni +255759374957**
**Mwl wa Taaluma +25575765268478**

**NDUGU MZAZI/MLEZI WA**……………………

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI LUPALILO HALMASHAURI YA MAKETE
MKOA WA NJOMBE MWAKA WA MASOMO 2026/2027

**YAH MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI LUPALILO HALMASHAURI YA MAKETE**

**MKOA WA NJOMBE MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2025/2026 kwa tahasusi ya ……………………………………(Jaza)
   Shule ya Sekondari Lupalilo ipo Mkoa wa Njombe wilaya ya Makete mji mdogo wa Ikonda km 80 kutoka Njombe mjini usafiri wa mabasi upo kuanzia saa 12 asubuhi hadi 12 jioni. Pia kwa upande wa Mbeya km 126 kutoka uyole hadi ikonda shule ilipo, usafiri wa mabasi kuazia 12 asubuhi hadi saa 7 mchana. Ukifika Ikonda sitendi na utapanda bodaboda hadi shule kwa tsh 3,000.
   **Mbeya** **uyole**
   Muhula wa masomo kwa kidato cha tano unaaza tarehe 8/07/2025 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ……………… na mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………………..
   Mzazi unatakiwa kuonyesha ushirikiano wa hali ya juu kwa walimu katika maendeleo ya mwanao kitaaluma kitabia na mwenendo wake kiujumla.
   Uvunjaji wa sheria, kanuni na taratibu za shule hautavumilika kamwe kama vile kumpa mwanao simu ya mkononi.
   Tafadhali soma maelezo yaliyoambatanishwa na barua hii uyaelewe na kuyatekeleze kisha jaza fomu zilizoambatanishwa na kuziwasilisha shuleni wakati wa kumleta mwanao kuanza masomo

## 2. MAMBO MUHIMU YAKUZINGATIA

Yafuatayo ni mahitaji/maagizo/michango na vifaa muhimu ambayo ni lazima uje nayo siku umletayo mwanao/mwanafunzi hapa shuleni.

### 2.1 SARE ZA SHULE (NGUO RASMI ZA SHULE)

1) Sketi moja ndefu ifike hadi chini kweye enka mshono wa linda box kitambaa Kizito rangi ya darkblue.( ISTIM NAMBA 1)
2) Mashati mawili meupe au zaidi ya mkono mirefu kwa ajili ya kuvalia sketi.
3) Kwa Yule atakaye chaguliwa kwa masomo ya sayansi anatakiwa kuwa na koti jeupe kama wanalovaa madaktari.(CBG,PCB na PCM)
4) T-shirt moja yenye nembo ya shule yenye rangi ya dark blue inapatikana karibu na mazingira ya shuleni.
5) Sweta mbili za rangi ya kijani jeshi.
6) Viatu vya ngozi jozi mbili rangi nyeusi ( vya kamba) , soksi jozi tano nyeupe ndefu.
7) Gauni Moja refu linalofika chini mkwenye enka kitambaa kizito (shamba dress) rangi ya dark blue (mshono wa solo) mikono mirefu.
8) Track suit moja nyeusi ufito mweupe pembeni isiyobana.
9) Jezi nyeupe kwa ajili ya mazoezi,(bukta na t-shirt yake) yenye/ maandishi ya TANZANIA kifuani ( TAIFA STARS).
10) Jacket zito jeusi lisilo na kofia nyuma na lisiwe na maandishi au urenbo wowote, kwa ajili ya kujihifadhi na baridi nyakati za usiku wakiwa darasani kujisomea.
11) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.
12) Hijabu nyeupe kwa ajili ya darasani na nyeusi kwa ajili ya kushindia(sio juba na hii ni kwa waisilamu tu).

### 2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI

a) Godoro la sponji 2.5 X 6, likiwa katika folonya
b) Vyombo vya chakula(sahani/kontena ,bakuli,kijiko na kikombe)
c) Mashuka mawili (2) ya rangi ya pink, blanketi moja nzito, mto, foronya ya pink, taulo na ndala.
d) Flat file moja (1) kwa ajili ya kutunza taarifa za wanafunzi (hatutapokea fedha)
e) Ndoo mbili (2) ( moja kubwa na nyingine ndogo).

### VIFAA VYA DARASANI /TAALUMA

1. Daftari 12 counter book kwaya 3 au 4
2. Biki za kuandikia , penseli za kucholea, rula ndefu , mkebe na vifutio
3. Dikishonari 1( Engliah to English)
4. Jalada 1(flat file) moja kwa ajili ya kutunza taarifa zake binafsi
5. Vitabu vya masomo yake /tahasusi husika
6. Rimu 2 za A4 za karatasi aina aina ya (aOne) kwa ajili ya mitihani ya wiki na mwezi.
7. Scientific calculator 1 f(x) 991 (kwa wale wanaosoma EGM,CBG,HGE,PCM na PCB tu).

Dissecting kit, Miwani ya Maabara gogozi ,pamoja na boksi moja la gloves kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi mwenyewe wakati wa masomo ya vitendo(hii ni kwa wale wanaosoma CBG na PCB tu.

**Mzazi unaweza kununua vitabu mbalimbali vya sekondari kwa ajili ya mwanao kujisomea kama una uwezo huo lakini sio lazima.**

## VIFAA VYA KAZI NA USAFI

1. PCM -Jembe moja jipya lenye mpini Na fagio la (chelewa) na moper 1
2. PCB- Moper 1, Fagio moja la (chelewa ) na fagio ( soft bloom) 1
3. CBG- Fyekeo ( slesha) 1, fagio moja la ( chelewa) na Moper 1
4. HKL- Brush hard blooms1, fagio moja la ( chelewa) na fagio ( soft bloom) 1
5. HGL-Blashi ya sink(kishungi) 1 na fagio moja la ( chelewa) na Moper 1
6. HGK-Moper 1 , fagio moja la ( chelewa) na hard bloom 1
7. HGE- Fagio (soft blooms) 1 na fagio moja la ( chelewa) na Moper 1
8. EGM- Jembe moja jipya lenye mpini Na fagio la (chelewa) 1
9. HGfa- Panga jipya 1, fagio moja la ( chelewa) na hard bloom 1

## 2.3: MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE

1) Mchango wa Uendeshaji wa shule 65,000/=
2) Tahadhari Tshs 5,000/=
3) Nembo ya shule 5000/=
4) Kitambulisho Tshs 5,000/=

**Jumla ya michango yote Tshs 80,000/=**

**Muhimu**

Mzazi/ mlezi hakikisha una mwandaa mwanao kikamilifu kwa mujibu wa maelezo na maelakazo yote ili kuepuka usumbufu.

Fedha hizi zote ziingizwe kwenye akaunti yetu ya shule yenye majina

**LUPALILO SECONDARY SCHOOL FEE ACCOUNT (NMB) NAMBA 60401100033**

Orodhesha vitu utakavyokuwa umelipia kisha njoo na ( Bank Pay in slip) kwa ajili ya mhasibu kukuandikia lisiti ya shule. Andika jina kamili la mwanafunzi unayemlipia. Tafadhali hatutapokea fedha mkononi zingatia hii, usipo zingatia hili uongozi haupo tayari kupokea malalamiko yoyote kuhusu malipo kinyume na maelakezo.

**Tahadhari**

a) kama hutakua tayari kujiunga na shule hii au kama unasoma tayari mahali pengine tafadhari ujulishe uongozi wa shule ili nafasi yako ichukuliwe na watu wengine wenye uhitaji.

b) Usipotoa taarifa ndani ya siku kumi na nne uongozi wa shule utatoa taarifa kwa kamati ya uchaguzi na nafasi yako itachukuliwa na watu wengine.

c) Shule hairuhusu kabisa nguo za nyumbani, zaidi uje na kanga na kitenge kwa ajili ya dharura yako binafsi, mara ukifika hapa shuleni tutakagua kikamilifu, njoo na nguo ambazo tumekuorodheshea, hapa si mahala pa kuonyesha mavazi ila ni mahala pa kusoma tu.

**Agizo:** Wakati wa likizo mwanafunzi atakaposafiri kurudi nyumbani kwao au kuja shule akiwa katika sare ya shule.

## 3.Sheria na kanuni muhimu za shule

3.Sheria na kanuni muhimu za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25. ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Technolojia yenye dhamana ya elimu na ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na.

## 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi,wazazi wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahusiano mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation); iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuvaaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, na
i. Mwanafunzi huruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwezako kubadili dini wawapo shuleni.

## MAELEZO MUHIMU

a) Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi
b) Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala katika kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
c) Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibari maalum toka kwa mkuu wa shule(Msiba au Ugonjwa).
d) Baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kutelekeza watoto wao bila kuwapa mahitaji muhimu ya fedha za matumizi wakiwa hapa shuleni, hivyo kuleta usumbufu kwa shule wakifikiri shule ina utaratibu wa kuwapa fedha wanafunzi , jambo ambacho ni jukumu la mzazi/mlezi
e) Baadhi ya wanafunzi wamekuwa na tabia ya kukataa kufanya kazi za nje kama usafi wa bweni kufyeka n.k shule haitavumilia tabia hiyo wala haitakuwa na huruma kwa wanafunzi wa aina hii, mwanafunzi ni lazima afundishwe elimu ya kujitegemea na hii ndiyo sera ya taifa letu.
f) Siku ya kumleta mwanao shule hutaruhusiwa kuingie bwenini bila kuripoti ofisi ya mkuu wa shule kwanza.
g) Bank Pay in slip zote ziwasilishwe kwa Mhasibu wa shule hapa Lupalilo Sekondari na siyo mahali pengine ili aweze kukuandalia stakabadhi yako ya kukiri kupokea fedha yako.

h) Sare ya shule ni lazima ivaliwe wakati wote wa masomo na kwenye shughuli rasmi kama vile mkutano, maandamano n.k uvaaji wa sare ya shule haitakiwi kuchanganywa na mavazi mengine wakati wote uwapo shuleni.

i) Maagizo ya fedha (michango ya shule) na mahitaji yote muhimu vyote vitakaguliwa mara tu mwanafunzi anapojiunga na shule hii.

j) Ni marufuku kuja na , hereni , mikufu na mapambo mengine pamoja na mitindo ya nywele isiyofaa. Shule hairuhusu kusuka mara zote uwapo shuleni utanyoa nywele zako . k)

**AFYA**

Unatakiwa kupima afya yako kabla ya kuripoti shuleni.Fomu maalum imeambatanishwa kwa ajili hiyo na utatakiwa kukabidhi fomu hiyo iliyokamilika mara tu ufikapo shuleni.kama una matatizo ya muda mrefu ya kiafya tafadhari toa taarifa mara ufikapo shuleni ukiambatanisha na vyeti vya hospitali. Shule haina uwezo wa kuhudumia mwanafunzi mwenye matatizo kwa chakula maalum. Shule pia haitavumilia mwanafunzi anayesingizia ugonjwa kwa sababu zake binafsi.

**UHURU WA KUABUDU**

Utaruhusiwa kuabudu kadiri ya dini na kwa kufuata sheria,ratiba na utaratibu wa shule, hivyo basi tabia ya kubughuzi wengine haitavumilika . shule haina dini ila watu wake wana dini na uhuru wa kuabudu, hivyo shule haitakubali/ wala kuvumilia tabia zozote za ubaguzi wa dini au ubaguzi mwingine wowote.

**KUBADILI JINA**

Haitaruhusiwa kubadili jina lako uwapo shuleni , litatumika kama lilivyotumika katika mtihani wako wa kidato cha nne (4) au kama lilivyo katika Selform yako ili kupunguza usumbufu wa usajili kwa mtihani wako wa kidato cha sita katika kipengele hiki mwanafunzi anaporipoti anatakiwa kuja na nakala/photocopy ya vyeti vyake vifuatavyo.

1. Leaving certificate 2. Result slip 3. Birth certificate(cheti cha kuzaliwa)

**3.2 MAKOSA AMBAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo mfululizo zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa
iii. Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzake, walezi na wakubwa. iv. Kugoma au kuhamasisha migomo.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi au kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
vi. Kufuga ndevu
vii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
viii. Uasherati ,uhusiano au kutoa mimba
ix. Kuoa au kuolewa
x. kusanabisha mimba au kumpa mimba msichana)
xi. Kutembelea majumba ya starehe au guest house

xii. Ulevi/madawa ya kulevya (kutumia au kukutwa nayo)

xiii. Kudharau bendera ya taifa. xiv. Kumiliki kukutwa au kutumia simu ya mkononi xv. Kutoka mipaka ya shule bila kibali. xvi.Uharibifu wa mali za umma kwa makusudi.

## OFISI YA WAZIRI MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## LUPALILO SEKONDARI
LUPALILO SEKONDARI TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi__________________________

Utaifa_____________________________ 

Dhehebu………………………………………………………

Mahali alipozaliwa……………………………………………

Anuani ya nyumbani…………………………………………

PASPORT SIZE YA MWANAFUNZI

2. Jina kamili la baba………………………………………………

Kabila………………………………………………… Dhehebu…………………………………………………

Umri…………………………………………..

Kazi……………………………………………

Namba ya simu…………………………………………

PASPRT SIZE YA BABA

3. Jina kamili la mama…………………………………………

Kabila……………………………………………………..

Dhehebu…………………………………………………..

Umri……………………………………………………….

Kazi………………………………………………………

PASPORT SIZE YA MAMA

Namba ya simu……………………………………………… 4. Jina kamili la mlezi(kama hauna wazazi)……………………………………………..

Kabila…………………

Dhehebu………………… Umri……………………..

Kazi……………………… Namba ya simu……………………… Uhusiano……………………………..

PASPORT SIZE YA MLEZI

5. Je wewe unaishi na nani?jina…………………………………………………………

Uhusiano……………………………………….

Anuani ………………………………………………..

PASPORT YA UNAISHI NAE

6. Je umewahi kuwa kiongozi? NDIO/HAPANA. Kama ni NDIO taja nafasi ipi…………………………………….

NDIO/HAPANA

NDIO

7. Utakuwa unakwenda wapi wakati wa likizo?..................................

(wakati wa likizo unatakiwa kwenda kwa mzazi au mlezi alietajwa hapo juu tu.kama utabadilisha mahali pa kwenda likizo mzazi/mlezi atoe idhini kwa maandishi mwezi mmoja kabla)

8. Taja ndugu watatu (3) wanaoweza kuja kukuona shuleni.Bandika picha (pasport size) zao hapa chini na utaje uhusiano wako na wao.

1.________________________________________________

2.________________________________________________

3.________________________________________________

**NB; Fomu hii ijazwe kikamilifu na mwanafunzi aje nayo siku ya kuripoti shuleni na itawekwa kwenye faili lake**

**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

LUPALILO SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 51,
MAKETE
13.05.2026

TO THE MEDICAL OFFICER …………………………………………………………………………

**PART A**

Please examines the above named pupils as to her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examinations should include the following categorises 1.Haemoglobin ……………………………………………….

2.P.V bleeding ……………………………………………………

3.Eye sight …………………………………………………………….

4.Blood pressure …………………………………………………………….

5.Urine and sugar ……………………………………………………………

6.Stool for routine examination …………………………………………………

7.Asthma …………………………………………………………..

8.Skin diseases ,…………………………………………………..

9.Epilepsy ……………………………………………………………………

10.Any deformity ……………………………………………………..

11.Pulmonary tuberculosis ……………………………………………

12.Neurosis …………………………………………………………………..

13.Venereal diseases ………………………………………………

14.Leprosy …………………………………………………………………

15.Other serious disease …………………………………………….

16. Pregnancy ……………………………………………………..

………………
JOHNES B LIOMBO
HEAD OF SCHOOL

**PART B**

(To complete by government medical officer)

1. I have examined the above named pupil and consider that she is physical and mental fit/ unfit for full time schooling. 2. Other comments ………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

**Name** …………………………………………………… **signature** ……………………

**Official stamp** ………………………………………… **Designation** …………………….

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
(TAMISEMI)
SHULE YA SEKONDARI LUPALILO

(TAMISEMI)

**SHULE YA SEKONDARI LUPALILO**

**FOMU YA MAPATANO/ KUKUBALI KUSOMA KATIKA SHULE YA LUPALILO SEKONDARI KIDATO CHA TANO MWAKA 2026/2027**

FOMU YA MAPATANO/ KUKUBALI KUSOMA KATIKA SHULE YA LUPALILO SEKONDARI KIDATO CHA TANO MWAKA 2026/2027

Kabla ya kusaini soma kwa makini maagizo yote. Shule haitapenda usumbufu wa aina yoyote ile usio na msingi.

JINA LA MWANAFUNZI/MLEZI ÷___________________________________________________

JINA LA MWANAFUNZI/MLEZI

KIDATO________________________________MCHEPUO_______________________

KIDATO:__________________ MCHEPUO_____

ANWANI:__________________MKOA/WILAYA___________SIMU YA MZAZI /MLEZI______________

ANWANI MKOA/WILAYA___________SIMU YA MZAZI /MLEZI

MIMI (Mwanafunzi) ____________________________________________________

MIMI :(Mwanafunzi)

Nimekubali /sikubali kujiunga na jumuiya ya shule ya Sekondari Lupalilo Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa , nahidi kuwa mtiifu na kuzingatia sheria , taratibu za shule kinyume chake hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwa pamoja na kufukuzwa shule.

Naahidi kusoma kwa bidii masomo yangu na kufaulu mitihani itakayotolewa na shule, wilaya mkoa na taifa.

Sahihi ya mwanafunzi ________________________Tarehe _________________________________

Mimi Mzazi/ mlezi wa mwanafunzi ________________________..wa kidato cha_________mwaka__________

Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa mtoto wangu nimekubali / sijakubali __________________mwanangu achukue nafasi hiyo.

Nahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia, pia na ahidi kumpatia mahitaji yote muhimu, matibabu na michango mingine mbalimbali tutakayokubaliana katika vikao vyetu vya wazazi na shule kwa wakati muafaka , kinyume na hapo nichukuliwe hatua za kisheria.

Sahihi ya mzazi / mlezi __________________________________

NB.Fomu hii itawekwa kwenye jalada la mwanafunzi kwa kumbukumbu zaidi

_____________________

**JOHNES .B. LIOMBO**

**(MKUU WA SHULE**

JOHNES .B. LIOMBO

(MKUU WA SHULE

**ORODHA YA VITABU MUHIMU KWA KILA SOMO**

ORODHA YA VITABU MUHIMU KWA KILA SOMO

Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma. Orordha ya vitabu vinavyotakiwa kwa kila idara ni kama ifuatavyo;

**TAMTHILIYA (KISWAHILI) (HGK&HKL)**

TAMTHILIYA (KISWAHILI) (HGK&HKL)

1. Mukwava wa Uhehe M.M.Mulokozi
2. Shujaa Mirambo EmmanuelMbogo
3. Usaliti Mjini FrancisImbuga

## USHAIRI (KISWAHILI) (HGK& HKL)

1. Fumbo Linaloelea NyambariC.M.Nyangwine
2. Malenga wa Ziwa Kuu WallahBinWallah
3. Andamo, Msafiri Safarini MohammedKhelefGhassani
4. Wosia wa Baba AhmedMohamedAmanzy

## RIWAYA (KISWAHILI) (HGK&HKL)

1. Dunia Uwanja wa Fujo EuphraseKezilahabi
2. Ua la Faraja W.E.Mkufya
3. Mirathi ya Hatari C.G.Mung'ong'o
4. Wasifu wa Siti binti Saad ShaabanRobert

## KISWAHILI (HGFa) USHAIRI

1. Utenzi Majumui wa Karne ya 21 IddM.Mwimbe
2. Dhifa EuphraseKezilahabi
3. Malenga wa Bara M.M.Mulokozi&K.K.Kahigi
4. Fungate ya Uhuru MohamedSeifKhatibu

## RIWAYA (FASIHI YA KISWAHILI) ( HGFa)

1. Vuta N'kuvute ShafiAdamShafi
2. Asali Chuungu SaidAhmedMohamed
3. Mwana wa Yungi MohammedSaidAbdulla
4. Vipuli vya Figo EmmanuelMbogo

## TAMTHILIYA (FASIHI YA KISWAHILI) ( HGFa)

1. Kaptula la Marx EuphraseKezilahabi
2. Nyerere na Safari ya Kanaan EmmanuelMbogo
3. Morani EmmanuelMbogo

# NOVEL (ENGLISH) HGL&HKL

1. Animal Farm GeorgeOrwell
2. Chasing the Leopard Finding the JulieWakeman-Linn
3. The Opportunist Elite NyambariC.M.Nyangwine
4. The Horizon Unveiled FellowesMwaisela

# PLAY (ENGLISH) HGL& HKL

1. The Government Inspector NicolaiV.Gogol
2. An Enemy of the People HenrikIbsen

3 . A Taste of Heaven FaroukTopan POETRY (ENGLISH)

## POETRY (ENGLISH) HGL&HKL

HGL&HKL

1. Summons: Poems from Tanzania RichardS.Mabalaetal.
2. Poets of Africa: Lament of the JaredAngira Silent & Other Poems

## MAVAZI YANAYOKUBALIKA KWA WANAFUNZI SHULENI









11